

# Mlinde Mtoto Wako dhidi ya Virusi Vikali vya Kupumua (RSV)

## Januari 2025


Virusi vya kupumua (Respiratory syncytial virus: RSV) ni virusi vya kawaida vinavyoathiri mapafu. Vinaweza kuwa hatari sana kwa watoto na wazee. Ni sababu kuu ya kulazwa hospitalini kwa watoto wachanga. Kwa bahati nzuri, kuna chaguzi mbili za kuwalinda watoto ugonjwa mbaya wa RSV, na watoto wengi wanahitaji moja tu: chanjo ya RSV inayotolewa wakati wa ujauzito au kingamwili ya RSV, inayoitwa nirsevimab, inayotolewa kwa mtoto. Mtoto wako mchanga anaweza kustahiki kupokea nirsevimab hospitalini baada ya kuzaliwa. Inatoa **ulinzi wa haraka** dhidi ya RSV na **hudumu angalau miezi mitano**.

Ikiwa unahitaji usaidizi wa kufikia au kuelewa maelezo haya, wasiliana na.

[ahs.vdhimmunizationprogram@vermont.gov](mailto:ahs.vdhimmunizationprogram@vermont.gov).

**Nirsevimab ina ufanisi wa 90% katika kulinda watoto wachanga kulazwa hospitalini na RSV kali.**

### Ukweli kuhusu RSV



- Msimu wa virusi vya RSV huanza katika Majira ya kupukutika kwa majani(Autumn) na hupanda wakati wa baridi(Winter).
- Vinaweza kuenea wakati mtu aliyeambukizwa anakohoa au anapiga chafya, kugusana kimwili na mtu aliye na virusi vya RSV, au kwa kugusa sehemu iliyoambukizwa.
- Watu wazima wengi walio na RSV hawana dalili zozote. Wale ambao wana dalili kwa kawaida watakuwa na ugonjwa mdogo, unaofanana na mafua.
- Watoto wachanga walio na RSV karibu kila mara huonyesha dalili. Hizi ni pamoja na kuwashwa, kupunguka kwa shughuli, kunywa au kula kidogo, na kuacha kupumua (kusimama kwa kupumua kwa zaidi ya sekunde 10).
- RSV inaweza kusababisha ugonjwa mbaya kwa watoto wachanga na watoto wadogo kama vile bronchitis (kuvimba kwa njia ndogo ya hewa kwenye mapafu) au nimonia (maambukizi ya mapafu).

### Kingamwili cha RSV (Nirsevimab)



**HealthVermont.gov/RSV**  
**802-863-7200**





- Kingamwili cha RSV hutolewa kwa risasi moja(sindano moja).
- Inapendekezwa kwa watoto wachanga walio chini ya umri wa miezi 8 ambao tayari hawajalindwa kupitia chanjo ya uzazi ya RSV. Vinatolewa kwa watoto wakati wa miezi ya Oktoba hadi Machi.
- Madhara kawaida huwa hafifu na huisha haraka.